

MWINGILIANO WA MAFUMBO NA MAUDHUI YA UONGOZI KATIKA NYIMBO ZA SITI BINTI SAAD

BY

JUMA NYONGESA JOB
CHUO KIKUU CHA PWANI



Article History

Received: 14/01/2023

Accepted: 18/01/2023

Published: 20/01/2023

Corresponding author:

JUMA NYONGESA JOB

Ikisiri

Makala hii ilichunguza Taarab hususani tungo za Siti Binti Saad. Kipengele cha Mtindo ambacho kiliangaliwa katika utafiti huu ni mafumbo. Vilevile, tumeangalia jinsi mafumbo yanavyoendeleza maudhui na dhamira katika utunzi wa nyimbo za Siti Binti Saad. Aidha, tumefumbua mafumbo mbalimbali katika nyimbo hizi. Suala la mafumbo na mandhari pia limejadiliwa kwa kina. Je, mandhari yana athari yoyote katika mafumbo ya Siti Binti Saad? Swali hili limeibua swali jingine – je, mafumbo ni jambo la mwandishi au jamii? Haya maswali yemejibiwa katika mawasilisho ya uchanganuzi wa data. Huu ni utafiti wa mtindo katika nyimbo za Taarab na umefanywa kwa kuzingatia mihimili ya nadharia ya Mtindo na ya Semiotiki. Nadharia ya Mtindo iliasisiwa na Buffon katika mwaka wa 1930 na kuendelezwa na Coombes na Leech katika mwaka wa 1969. Mtindo unahusu jinsi mtunzi anavyojieleza kwa kutumia lugha. Mtindo ni muhimu sana katika kazi yoyote ya fasihi kwa kutokana na mchango wake katika kuwasilisha ujumbe. Utafiti ulifanywa maktabani, nyanjani na kwenye wavuti. Data ilituliwa kwa njia ya nasibu na kimakusudi kwa sababu ililenga mtribu mmoja ambaye nyimbo zake zinajulikana tayari. Aidha, tulitumia mahojiano, vitabu, makala mbalimbali na tasnifu za watafiti wengine ili kutoa maelezo zaidi kuhusu data. Ilijitokeza kuwa mafumbo husaidia katika kuwasilisha mawazo au hisia za mtu kwa njia ya upole bila kuleta mhemko au mabishano baina ya watu. Ni njia moja ya kusema bila makali ya maneno. Isitoshe, ilidhihirika kuwa mafumbo ni njia mojawapo ya mitindo yauimbaji wa Taarab ya asili.

Maneno muhimu: Ufakiri, mafumbo, usawiri, dhuluma na utabaka

Utangulizi

Uongozi huhusisha uajibikaji kwa yeyote yule aliye na jukumu la kutekeleza katika jamii. Iwapo mja atatekeleza jukumu hilo vizuri huchukuliwa kuwa mwenye uongozi mzuri naiwapo atafeli kutekeleza wajibu huo hurejelewa kama mwenye kufeli katika uongozi. Malezi vilevile, huhusisha uajibikaji wa wazazi kwa wana. Uongozi na malezi katika jamii ya Unguja ni masuala ambayo Siti aliliangazia katika nyimbo zake. Siti alibua hali hiikwa ufundi wa mafumbo. Mafumbo aliyotumia Siti yalibeba jumbe za kudhihirisha hali halisi ya uongozi katika jamii ya Unguja.

Yalioandikwa kuhusu mada

Masuala mengine yaliyopata kushughulikiwa katika Taarab ni pamoja na mtindo. Wasomi Njogu na Chimera (1999), wanakiri

kuwa hakuna njia moja ya kueleza mtindo. Kwa jumla, wanasema kuwa mtindo ni tabia ya utungaji inayopambanua baina ya mtunzi mmoja na mwingine. Wafuata Njogu (2007), wanaeleza kuwa madhumuni ya msanii hayawezi kutenganishwa na jinsi msanii huyo anavyoiwasilisha kazi yake. Wanasema kuwa kadiri mwanafasihi anavyowaza ndivyo vipengele mbalimbali vya kuwazia vinavyomjia. Tunaafikiana na maelezo ya wataalamu hawa, ufiki wetu umetokana na uelewekaji kuwa, mafumbo yanahusisha fani na maudhui ambayo ni viungo muhimu vya fasihi na ambavyo haviwezi kutenganishwa vikaweza kujisimamia. Kahigi na Mulokozi (1982), wanasema kuwa kanuni kuu katika utunzi wa mashairi ni uwiano kati ya fani na maudhui. Kwao, kanuni hii ndiyo inayoweza kuwa ‘roho’, ‘uti’ wa mgongo’ wa ushairi na fasihi kwa jumla. Kazi ya Kahigi na Mulokozi (washatajwa) iliawezesha watafiti kupata pengo la kutafitia. Utafiti huu ulilenga mtindo wa mafumbo tofauti na kazi ya Kahigi

na Mulokozi (washatajwa) ambayo ilizungumzia mitindo mbalimbali.

Mohamed (1995), ameeleza kuwa kazi ya kisanaa isiyokuwa na uzuri wa kisanaa huwa chapwa; kazi ya fasihi inayojengwa kwa 'majineno mitupu' inayodhaniwa inavutia huwa 26 nyepesi mno na haithaminiki kisanaa. Pindi maudhui fulani yanayomhusu mwanadamu, maisha, maendeleo na mashirikiano yake yataingia kwenye nadhari na hatimaye mikono ya msanii mzuri atayafinyanga vyema na kumfaa anayewasilishiwa kwa nguvu za aina mbili: nguvu za maudhui zenye uzito na nguvu za kisanaa zenye mvuto. Hali hii humfanya mwandishi wa aina hiyo, kuwa mwenye kufaulu zaidi kuliko yule ambaye ametumia nguvu za aina moja. Kazi hii itatufaa kwa kueleza umuhimu wa mtindo wa mafumbo kwa kazi ya fasihi ya Siti. Utafiti huu umejikita katika kipera mojawapo cha semi kwa jina mafumbo. Uelewaji wa mtoto huanza kwa kuelewa mzazi.

Juma (2016), anasema kuwa kwa kawaida semi katika lugha ya Kiswahili zinatumia lugha ya picha mbalimbali kama vile mimea, ndege, wanyama na viumbe vinginevyo. Picha hizi huwekwa kwa lengo la kumuwakilisha mwanadamu. Semi ni kielelezo cha dhamira ya Mswahili. Muundo wa Utafiti Utafiti huu ulichambuliwa kwa njia ya maelezo. Enon (1998:24), anaeleza kuwa njia ya maelezo ni njia ya uchambuzi wa data kwa hali ya ufafanuzi wa kawaida ambapo nambari hazitumiki. Kuna utafiti ambao hutumia data ya 'wingi idadi' na mwingine ambao hutumia uchunguzi wa udadisi wa 'kithamano', ambapo hesabu ya matukio au hulka yoyote haitiliwi maanani. Utafiti huu ulijikita katika mkabala wa maelezo ya kithamano ili mtafiti aweze kuchanganua sifa za ujuzi wa utunzi wa mafumbo wa msanii Siti Binti Saad. Sukamolson, (2010), utafiti wa kimaalezo unahusika na ufafanuzi kuhusu matokeo ya kijamii. Utafiti huu huwasaidia watu kuelewa ulimwengu wanakoishi na ni kwa nini mambo huwa jinsi yalivyo? Utafiti wa kimaalezo unahusu maoni, tajiriba na hisia za watu ambako data hukusanywa. Hali kadhalika utafiti wa kimaalezo hujikita kwenye vipengele 43 vya kijamii. Kwa mujibu wa Crossman (2020), utafiti wa kimaalezo ni utafiti wa kijamii unaotumia data ambayo si ya kitakwimu. Utafiti wa kimaalezo unalenga kufasiri maana kutoka kwa data kwa nia ya kuelewa maisha ya kijamii kupitia uchunguzi wa makundi ya watu kutoka maingiliano yao ya kila siku. Utafiti huu ulilenga kufasiri maana ya mafumbo yanayopatikana katika nyimbo za Siti Binti Saad.

Wimbo 'Ufakiri'

Siti anazungumzia kuhusu hali mbaya inayosababishwa na umaskini. Umaskini hufanyabinadamu kukosa kuthaminiwa na binadamu wenzake. Huchukuliwa kama tambara bovu. Hakuna mtu ambaye huwa anataka kuhusiana na mtu maskini. Jambo la ajabu ni kuwa, umaskini unaweza kumpata mtu yeyote katika dunia. Umaskini ni mojawapo ya majaliwa ya mwenyezi Mungu. Kwa hivyo, ni vyema watu kuwa wangwana na wastahimilivu kwawale wenzao ambao ni maskini. Siti alitaka kuwepo kwa usawa katika utangamano miongoni mwa wanajamii.

Umaskini unarejewa kama ufakiri katika lahaja ya Kiunguja. Msitari huu, 'ufakiri kama kiza hakina nuru' unasema kuwa umaskini ni kama giza na kwenye giza hakuna mwanga. Siti

alikusudia kuashiria kuwa mtu maskini huwa hana maono au mwelekeo wowote kuhusu maisha. Huwa ni kama mwendawazimu, hana uwamuzi wowote kuhusu mstakabali wa maisha yake. Siti anaendeleza kudharauliwa kwa mja maskini kwa kusema 'usemalo kama ndoto mwema hufanya ayari'. Siti alimaanisha kuwa mtu maskini hataakiwa mzuri huchukuliwa kama tambara bovu na hata akisema maneno yake huwahayatiwi maanani na yeyote yule. Huwa ni kama hana maana mbele ya watu. Mfano katika ubeti wa wimbo Ufakiri:

Ufakiri jambo zito aliloumba Kakhari

Mkubwa huwa mtoto na rijali huwa thori

Usemalo kama ndoto mwema hufanya ayari

Jamii nyingi aghalabu huwatenga watu ambao hawana chochote au maskini. Maskini huchukuliwa kama ombaomba katika jamii. Watu hawa hohehahe huishia kuishi maisha ya upweke. Hali hii inajitokeza kwa kauli 'jamii hufukuzwa na uwe mtu fakiri'. Mfano katika ubeti:

Jamii hufukuzwa na uwe mtu fakiri

Watu kukufanya nyani au hinzani

Sikutakabari walini haribu

Msitari wa 'watu kukufanya nyani au hinzani' una maana ya ndani. Nyani ni mnyama ambaye ni wa msituni na hufukuzwa na binadamu kwa sababu huwa ni mharibifu wamimea shambani. Siti alimaanisha kuwa jamii huchukulia vibaya watu maskini. Maskini huonekana kama wenye uharibifu kwa rasilimali.

Wimbo 'Mbembeze Mtoto'

Wimbo huu uliimbwa na Siti kama njia ya kutoa wasia kwa watoto wasichana. Siti anawashauri watoto wasichana kukubali kulindwa na wazazi wao ili baadaye waweze kufaulu maishani. Kuna hatua ngumu ambazo wanapitia ndiposa kuweza kufaulu lakini ni muhimu waweze kustahimili hayo yote. Siti anabashiri kuwa wakivumilia hali hizi ngumu wataishia kutuzwa na wazazi wao. Vilevile, Siti anawashauri kuwa wataweza kuposwa kwa familia zenye ufahari mkubwa kama za wafalme. Siti anamkataza motto asilie anapotibiwa kwa kijungu na ubani. Mtoto atalia wakati yeye mzazi wake atakapoagadunia. Msitari 'ina uombezi wangu nyota' una maana ya ndani. Mfano katika ubeti wawimbo Mbembeze Mtoto:

Howa, kibibie howa, ni

Kijungu na ubani

Dawa kuu ya mangani

Ina uombezi kwani

Uombezi wangu nyota

Na mwana wa Sultani

Howa bibie howa

'Nyota' ni kitu ambacho huwa ni cha kupendeza sana. Mtu akiwa na nyota huwa inamaana kuwa amebahatika na anaendelea vizuri katika maisha au jambo fulani. Sitialikuwa akimwombea yule mtoto wake abarikiwe na apate kufanikiwa maishani hasabaada ya kuingwa kwa dawa za kijungu na ubani dhidi ya mapepo.

Siti anatambulisha mbuzi na ng'ombe kuashiria zawadi ambazo mtoto huyu angepata baada ya kuwa mtiifu kwa wazazi wake.

Anasema kuwa 'nikupe kundi la mbuzi na ngombe unywe maziwa'. Zawadi hizi zingemuwezesha kufaulu maishani na kufurahia matunda ambayo ndiyo maziwa. Mbuzi na ng'ombe ni viwakilishi vya baadhi ya urithi ambao wazazi huachia watoto wao. Mafanikio ya urithi huu ndio 'maziwa'. Matunda yakufaulu maishani huwa ni mazuri sana kwa mtoto hata mzazi hufurahia mwanaweanapofaulu. Mfano katika ubeti:

*Kua bibie kua
Nikupe wasia
Nikupe kundi la mbuzi
La ngombe unywe maziwa*

Siti anaashiria kumzawadi shangazi yake kwa ushauri aliompaa. Anasema kuwa kuna 'kidau kijacho na kina mkufu'. Kuwepo kwa mkufu katika kidau ni ishara kuwa Sitiamefaulu maishani. Mkufu ni kitambulisho cha vitu vya thamani ya juu. Siti anasema kuwa zawadi hii atampa shangaziye kwa sababu ndiye aliyemshughulikia. Mfano katika ubeti:

*Kile kidau kijacho
Hamkosi mna changu
Mna mkufu nikupe
Kadiri ya shingo yangu
Siutupi siuvai
Wala simpimwenzangu
Tampa mama shangazi
Ajuaye siri yangu*

Ubeti huu ni fumbo tupu. Siti anazungumzia kuhusu bidii aliyokuwa ameiweka maishani mwake lakini hakuwa anafaulu. Uwepo wake karibu na ufuo ni ishara ya kutaka kuvukang'ambo nyingine lakini ameshindwa kwa kuwa kigalawa hakikuwa kinamsikiza. Sitaliishia kusikitika kwa kukosa kuvuka. Anasema kuwa, 'Ni nini hakika? Kando kando yamto, nakiita lakini hakiitiki. Kinanifanya nasikitika'. Baadaye Siti alifaulu kuvuka baadaya kusaidiwa na shangazi yake maishani. Mfano katika ubeti:

*Kile kidau kijacho
Hamkosi mna changu
Mna mkufu nikupe
Kadiri ya shingo yangu
Siutupi siuvai
Wala simpimwenzangu
Tampa mama shangazi
Ajuaye siri yangu*

Siti anaashiria kuwa baada ya kushughulika maishani alifaulu na sasa ana zawadi kwashangazi yake ambaye alielewa masaibu yake. Zawadi hii hakuna mtu ameiona ni yeyetu.

Wimbo 'Si mji haukaliki'

Nasra (2007:74), anasema kuwa kikundi cha Siti Binti Saad kilipoenda kutumbuizawafuasi wao katika kisiwa cha Pemba walikumbana na hali mbaya ya jiji la Jambang'omehuko Mgagadu. Sehemu hii ilitawaliwa na Mwarabu mmoja ambaye aliwafanyisha Waafrika kazi ya kijungujiko. Waafrika wengi waliuliwa na kurushwa kwenye shimoalilokuwa amelichimba Mwarabu huyu. Kufuatia kisa hiki Siti na kundi lakehawakufurahia na wakaunda

wimbo Si mji haukaliki. Siti anaibua hali ya mji kuwa natatizo kwa kauli 'si mji haukaliki una miba unachoma'. Mfano katika ubeti:

*Si mji haukaliki una miba unachoma
Na ahera hakwendeki tumetangulia dhima
Na mambo hayanyoki kula siku twalalama
Lipi sisi la salama hata tukarudi hali*

Miba huwa inamduru mtu hasa kwa kuumiza inapomdunga. Mara nyingi katika fasihimwiba hutumika kuashiria mtu hatari katika shughuli fulani. Siti katika wimbo huuanamuwasilisha mwarabu mkulima kama mwiba kwa kuwa anawatesa Waafrika kwa kaziya kijungu-jiko. Waafrika wazembe anawaua na kuwarusha kwenye shimo kubwa. Halihii ya kuwaua Waafrika inajitokeza kuwa hatari kwa jamii.

Siti ametumia taswira ya maji ambapo mtu akianguka majini anaweza kuelea akiwa anajuakuogelea au kuzama kama hajui. Anafumba hali hii kwa kusema kuwa 'kila uchao huzidihataelei tunazama'. Mfano katika ubeti:

*Kila tukijitahidi huona nyuma
Kila uchao huzidi hatuelei tunazama
Turehemu ya Wadudu mwenye wingi wa rehema
Lipi sisi la salama hata tukarudi hali*

Ukizama majini huna lako, wewe unaelekea jongomeo. Siti anailinganisha hali hii yakuzama na kuelea na maisha ya kawaida ambapo anatambua kuwa wakaazi wa Jambang'ome wameshindwa kujimudu katika maisha. Hali wanavyoendesha na Mwarabu mkulima imewashinda. Kushindwa huku kunasawiriwa kama kuzama. Maishaya huko Jambang'ome ni magumu sana kwao. Wanatumikishwa katika mashamba yajamaa huyu tajiri bila malipo yanayofaa. Wengine wanauliwa na kutupwa kwenye shimokubwa kwa kukataa kutumikishwa.

Mwimbaji anasema kuwa wao wemekata tamaa kwa hali hii ngumu. Kukata tamaakunajitokeza kwa kauli 'kila tukijitahidi huona nyuma'. Kuona nyuma ni kukosa kupatamwanya wa kujikomboa kutoka kwa lindi hili la Mwarabu mkulima. Siti anatambulishakuona nyuma kama kukosa matumaini kwa wakaazi hawa wa Jambang'ome. Siti anaashiria kuwa kazi hazipo katika mji ule ila zile zilizopo ni za sulubu. Anasema kuwa wao hawawezi 'kutweka na kusukuma'. Mfano katika ubeti:

*Zimeadimika kazi hapana ila likwama
Na sisi hatuiwezi kutweka na kusukuma
Turuzuku ya Azizi Mruzuku Umma
Lipi sisi la salama hata tukarudi hali*

Inaashiria kazi ngumu za ukulima katika shamba la Mwarabu huyu katili. Siti alikuwaakizungumzia hali ngumu ya maisha katika shamba la Mwarabu huyu katili. Kazi ambazozilipatikana zilikuwa ni za sulubu. Hali hii ya mateso ya watu wa Bungi inadhihirika kwa usemi wa ubeti ufuatao:

*Niliona mateso ya watu wa Bungi
Nguruwe dume imefungwa kwa msalaba
Bungi aliona kaburi la mtumwa*

Ubeti huu unaashiria kuwa Siti alipoenda kutalii ufuo wa Bungi aliona kaburi la mtumwa. 'Nguruwe dume' inaashiria mtumwa mwanamume ilhali msalaba inaashiria kaburi. Kwahivyo, Siti aliona kaburi la mtumwa aliyeuawa na Malkia wa Ufalme wa Bungi. Malikia huyu inaaminika alifanya mahusiano na watumwa hawa na mwishowe kuwauwa (Nasra, 2007:13). Mfano mwingine wa ubeti wenye maelezo ya uongozi wa Bungi:

*Kinakuja kijaluba kingine kikubwa
Kijaluba ambacho kina karafu ndani
Mwenye Kijaluba yuko vipi?*

Siti anatambulisha kuwa sehemu ile ya Bungi ni ukweli kuwa kuna ufalme mwingine. Anapotaja uwepo wa 'kijaluba ambacho kina karafuu ndani' ni ishara ya watu wa haibaya juu. Kijaluba kimetumika kutambulisha watu wa haiba au nafasi ya juu katika jamii. Siti katika wimbo huu anasema kuwa hicho kijaluba kinafurahisha sana. Anajiuliza kuwamwenye kijaluba yuko vipi?

Wimbo 'Kigalawa'

Wimbo huu ulitungwa kuashiria kuwa, maskini na tajiri walihitaji kutangamana bila matatizo yoyote. Binadamu wote wanahitaji hadhi na heshima. Siti na kikundi chake waliimba wimbo huu walipoalikwa kumtumbuiza Sultan Seyyid Khalifa na mke wake Bibi Matuka katika kasri lao Fair (2013:33). Siti anasema kuwa atatumia kigalawa kuvukang'ambo nyingine kumueleza mfalme masaibu yao ya kuwa watumwa. Amebeba mzigomdogo ambao angeutumia kulipia kama poni. Anakubali kulipia nusu pauni ili kujepushana shida ya utumwa. Anasema kuwa yeye atatumia vizuri rasilimali ambazo yuko nazo naanasema hakopeshi wala hauzi mali yake. Anaendelea kusema kuwa kazi yake ni kuliwazawale ambao wanalalama au kulia. Aliwahimiza wenzake wachochole watafute shughulimuhimu yakufanya ili wajitegemee waache kulalamika. Mafumbo katika wimbo wa Kigalawa:

Kigalawa ni chombo cha usafiri majini, Siti anajilinganisha na kigalawa. 'Kigalawa' kinaashiria watu wa tabaka la chini. Siti anaona kuwa kigalawa ni kidogo lakini piakiruhusiwe kusafiri baharini katika shughuli ya kuchuma mali. Hali ya wakaazi wa Ng'ambo ambako Siti alitoka ilikuwa ngumu sana na utabaka ulikuwa umewakandamizazaidi. Siti alikuwa akipigania haki ya watu wa tabaka la chini ili wawe huru wakichumamali yao. Mfano katika ubeti:

*Kigalawa sawa sawa na chombo
Baharini huenda mirengo mirengo
Sivuwani shuka ya sitiri mambo*

Siti anahusisha uwezo wa kigalawa na vyombo vingine vya majini. Anaona kuwa hatamaskini au watu wanyonge wana uwezo wa kuchuma mali. Kuwa na 'vitu ndani kwakigalawa' ndiyo kuchuma mali. Mali hii inaweza kutumika kulipia pauni. Siti anaashiri kuwa kigalawa kama vyombo vingine vya majini kina hadhi na thamani yake. Maskinipia wanahitaji kupewa heshima kwani wana thamani yao katika dunia. Tazama ubeti ufuatao:

*Kigalawa kumbe kina vitu ndani
Unitweke hata kwa mwinye Husseni
Japo moto sinitia kisimani*

*Kigalawa ulete mali kapuni
Ni tajiri takupa nusu pauni
Yangu ya mkufu upate kuweka poni.*

Maisha yao na watu matajiri ni sawa. Shida ambazo matajiri wanapitia maishani ndizomasikini wanakumbana nazo. Hali hii ya matatizo ya tabaka hizi mbili Siti alifumba kwakusema, 'baharini huenda mirengo mirengo'.

Siti anasema kuwa ni vyema kuwe na ushirikiano kati ya tajiri na maskini. Hali hii ikitokeajamii itanawiri vizuri. Siti anajenga ujumbe huu kwa kusema 'moto sinitia kisimani'. Mfano katika ubeti:

*Kigalawa kumbe kuna vitu ndani
Unitweke hata kwa mwinye Hussein
Japu moto sinitia kisimani*

Moto unatarajiwa kuangaza vizuri kisimani ili shughuli ziendelee lakini iwapo hakunamaelewano basi moto utazimwa na maji ya kisima. Moto ukizimwa shughuli zitagongamwamba kwa kukosekana mwangaza.

Wimbo 'Ela kafa ndugu zangu'

Wimbo huu unazungumzia visa vya wizi katika nchi ya Zanzibari wakati wa ukoloni. Wakati wimbo huu ukivuma kulikuwa na kisa cha kachero wa serikali ya Uingereza aliyekuwa amefungwa na kutumikia kifungo cha kazi ngumu. Kachero huyu alikuwa amewaibia Wakoloni pesa zao ili kuandaa sherehe ya kuzaliwa kwa mwanawe, akakamatwa na kushtakiwa. Aliambulia kushindwa na kutumikia kifungo cha jela. Alionekana akibeba jiwe zito kichwani (Fair, 2013:38). Kachero huyu alijulikana kama Bwana Mselem.

Siti katika wimbo huu anawaonya ndugu zake wa mashambani kuwa wizi ni tabia mbayana ni hatari. Anawaeleza kuwa wasidanganywe kuwa kuna suala la rufaa katika wizi. Anawashauri wasisikize mahakimu waliosomea Landani, ni matapeli. Siti alikemea wizi wa makachero pia na maofisa wengine wa serikali ya ukoloni. Tazama ubeti ufuatao wawimbo *Ela kafa ndugu zangu*:

*Ela kafa ndugu zangu wa shamba hata mjini
Mwenye kazi za mzungu maliki wa duniyani
Roho mzipige rungu cha mtu msitamani
Msitamani...*

Siti anaashiria kukomesha roho za tamaa kwa kusema kuwa 'roho mzipige rungu, cha mtumsitamani'. Kukataa majaribio ya tamaa ndiyo kupiga roho rungu. Anawashauri kukomakudanganywa kuhusu wizi wa mali ya wenyewe. Wakili aliyesomea Landani Siti anaonakuwa wananawiri kwa sababu ya tamaa ya wakaazi wa Unguja. Mwimbaji anasema kuwawakili 'aikaze suruali'. Mfano katika ubeti:

*Wala haifai wakili aliyesoma Landani
Bure ataila mali upeleke gerezani
Aikaze suruwali akimbiliye nyumbani
Akimbiliye nyumbani...*

Fumbo hili linaashiria kuwa wakili aliyesomea Landani ataweza kunufaika na kunenepa kwa kukuhadaa ilhali kesi itakuwa na

mapendeleo. Kesi ya wizi itaamuliwa kuegemea upande wa serikali. Juhudi zozote zitashindwa. Muhimu anawaomba kuepuka na wizi wamali ya wenyewe. Mwimbaji anasema kuwa 'halipo la manufaa ikishapita saini'. Mfanokatika ubeti:

*Msishikwe na tamaa kama ipo rufaani
Hiyo ni ya hadaa mjitiye mitegoni
Halipo la manufaa ikishapita Saini
Ikishapita saini...*

Hakutakuwa na manufaa iwapo kesi ishaamuliwa. Watu wa tabaka la chini hawana uwezomwingine hakimu akishaamuwa kesi. Kuwekwa saini ndiko kuhukumu kwa kesi. Sitanazidi kusema kuwa uamuzi wa hakimu huwa na mapendeleo ya kitabaka. Wale watabaka la juu hufaidi katika maamuzi yake. Uamuzi wa hakimu ambao hufanywa mezanihuwa ni wa kupendelea. Iwapo unatoka katika tabaka la chini uwamuzi huwa ni wakukandamiza. Lakini iwapo unatoka tabaka la juu uamuzi huwa unaegemea upande waserikali. 'Jiti la ncha jichoni' inaashiria kuwepo na upendeleo katika maamuzi ya hakimu. Mfano katika ubeti:

*Msicheze na Hakimu ahukumuye mezani
Bure mtajidhulumu kwa ajili kitu duni
Na haya mwayafahamu, jiti la ncha jichoni*

Kiishio

Makala hii imedhihirisha wazi kuwa mafumbo hukuza maudhui. Huweza teganisha maudhui na mtindo. Vitu hivi viwili haviwezi teganishwa. Ni kama mgongo na uti. Siti alipania kuzungumzia uongozi na dhuluma kwa njia ya mafumbo. Aliweza kuwasilisha mawazo yake kwa njia ya upole bila makali. Mafumbo yalimwezesha Siti kuwasema wakubwa wake kwa njia ya uhuru bila uoga. Makala haya yamesisitiza umuhimu wa mtindo katika kazi za fasihi.

MAREJELEO

1. Abdalla, A. R. (2018). *Kuchunguza Dhamira na Fani katika Nyimbo za Taarab Asilia: Mifano ya Nyimbo za Shakila Saidi Khamisi [Masters, The Open University of Tanzania]*. <http://repository.out.ac.tz/2020/> (haijachapishwa)
2. .Abdi-Jalebi, A. (2018). *Fasihi Simulizi katika Jamii. Mulika 2: 34-44.*
3. Acquaviva, G. (2004). *Jazanda ya Njozi katika Baadhi ya Mashairi ya Euphrase Kezilahabi. Swahili Forum 11: 69-73.*
4. Adam, O. A. (2014). *Kuchunguza Dhamira za Kijamii na Kiutamaduni Katika Riwaya ya*
5. *Kiswahili: Mifano Kutoka Kuli na Vuta N'kuvute [Phd, The Open University of Tanzania]*. <http://repository.out.ac.tz/434/> (haijachapishwa).
6. Haji, A. (1935). *Al-Faraid Al Durriya. El- Macheroq Beirut Lebanon.*
7. Ahmed, M. (2005). *Taarab in Zanzibar. Nordic Journal of African Studies 14,3: 356-367*
8. Akaranga, S. I., & Makau, B. K. (2016). *Ethical Considerations and Their Applications to Research: A case of the University of*

- Nairobi. http://erepository.uonbi.ac.ke/handle/11295/100502 (haijachapishwa).*
9. Alawi, Z. M. (2007). *Nyimbo za Taarab Zinavyochangia Kudumisha Maadili ya Wanzanzibar. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Tanzania (haijachapishwa).*
 10. Alhabibu, E. A. (2012). *Matumizi ya Lugha katika Nyimbo za Taarab. Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu cha Tanzania. http://repository.out.ac.tz/2913/1/TASNIFU%20YA%20ASHA%20RAMADHANI%20ALI.pdf (haijachapishwa).*
 11. Ali, A. E. (2014). *Kutathmini Nafasi ya Mwanamke katika Mashairi ya Kiswahili: Uchunguzi wa Mashairi ya Shaaban Robert na Mathias Mnyampala [Masters, The Open University of Tanzania]*. <http://repository.out.ac.tz/534/> (haijachapishwa).
 12. Ali, A. H. T. (2014). *Taashira na Utendaji katika Nyimbo za Harusi za Waswahili. Kisiwani Unguja [PhD Thesis]. Egerton University (haijachapishwa).* 190
 13. Ali, H. B. (2018). *Wahusika wa Kimimi katika Riwaya ya Kiswahili: Mifano kutoka Dunia yao na Nyuso za Mwanamke. http://repository.udom.ac.tz/handle/20.500.12661/1002 (haijachapishwa.)*
 14. Al-Qaradawi, Y. (2002). *Abdulaziz, MH, Muyaka: 19th century Swahili Popular Poetry, Nairobi: Kenya Literature Bureau, 1979. Abun-Nasr, Jamil, 'Islamisches Recht innigerianischen Rechtssystem', in Muslime in Nigeria: Religion und Gesellschaftim politischen Wandel seit den 1950er Jahren, Abun-Nasr, Jamil (ed.), MünsterHamburg: Lit-Verlag, 1993. Perspective, 61(2), 251-268.*
 15. Anasiudu, O. (2020a). *Stylistics: Theory and Practice, Ikenna Kamalu. 11, 1-7. https://doi.org/10.25159/2663-6565/7039*
 16. Anasiudu, O. (2020b). *Stylistics: Theory and Practice, Ikenna Kamalu. Imbizo :International Journal of African Literary and Comparative Studies, 11(1), 1-7. https://doi.org/10.25159/2663-6565/7039*
 17. Arasa, A. E., Omari, O. J. & Nancy, A. (2017). *Mchango wa Mazingira ya Mwandishikatika Matumizi ya Mafumbo. International Journal of Arts and Education. 1: 1-17. http://localhost:8080/xmlui/handle/123456789/7168*
 18. Askew, K. (2002a). *Performing the Nation: Swahili Music and Cultural Politics in Tanzania. University of Chicago Press. https://press.uchicago.edu/ucp/books/book/chicago/P/bo3637399.html*
 19. Askew, K. (2002b). *Performing the Nation: Swahili Music and Cultural Politics in Tanzania. University of Chicago Press. https://press.uchicago.edu/ucp/books/book/chicago/P/bo3637399.html*
 20. Askew, S. (Ed.). (2000). *Feedback For Learning. Routledge. https://doi.org/10.4324/9780203017678*
 21. Babbie, E. R. (2001). *The Practice of Ssocial Research. Wadsworth Thomson Learning. 191*

22. Badru, Z. A. (2021). *Taswira na Mabadiliko ya Kiujumi katika Vitendawili vya Kiswahili*. *Mulika Journal*, 39(0), Article 0. <http://196.44.162.39/index.php/mj/article/view/4021>
23. Bakhtin, M. M. (1990). *Language, Literacy and Learning*. Cambridge University Press.
24. Bailey, R. (2003). *Conceptual Metaphor, Language, Literature and Pedagogy* (Vol. 1). <https://studylib.net/doc/8032455/conceptual-metaphor--language--literature-andpedagogy>
25. Bailey, T. R. (2003). *A Researcher's Perspective*. *New Directions for Community Colleges*, 2003(122), 93–100. <https://doi.org/10.1002/cc.114>
26. Balisidya, M. L. (1987). *Tanzu na Fani za Fasihi Simulizi*. *Mulika*, 19, 2–10.
27. Barthes, R. (1994). *The Semiotic Challenge*. University of California Press.
28. Beauchamp, T. L., Beauchamp, P. of P. and S. R. S. at the K. I. of E. T. L., Childress, J.F., & Childress, U. P. and H. P. of E. J. F. (2001). *Principles of Biomedical Ethics*. Oxford University Press.
29. Broughton, S., Ellingham, M., & Trillo, R. (1999). *World music: The Rough Guide*. *Rough Guides*; Distributed by the Penguin Group.
30. Brunotti, D. I. (2012). *Ngoma ni Uhuni? Swahili-Forum* 12:20-35.
31. Buffon, R. (1930). *Research Geneology 1872-1930—Ancestry®*. <https://www.ancestry.com/genealogy/records/richard-priestly-buffon-24-fdvst>
32. Carter, R., & Simpson, P. (2003). *Language, Discourse and Literature: An Introductory Reader in Discourse Stylistics*. Routledge.
33. Coombes, H. (1953). *Literature and criticism*. London,: Chatto and Windus. <http://archive.org/details/literaturecriticoom>
34. Crossman, A. (2020). *What Is Qualitative Research?* ThoughtCo. <https://www.thoughtco.com/qualitative-research-methods-3026555>
35. Chai, F. (2003). *Gaining Access in Fieldwork*. Makala iliyowasilishwa katika Warsha ya 192 AICD Idara ya Lugha na Isimu, Chuo Kikuu cha Egerton tarehe 15/11/2003.
36. Cuddon, J. A. (2017). *The Penguin Dictionary of Literary Terms and Literary Theory*. <http://archives.unc.edu.dz/handle/123456789/111184>
37. Dinesh, K., & Mehta, M. (2002). *British National Formulary, Number 43 BennettBooksLtd*. <https://www.abebooks.com/9780853695103/British-NationalFormulary-Number-March-0853695105/plp>
38. Druckman, D. (2005). *Doing Research: Methods of Inquiry for Conflict Analysis—UQeSpace*. <https://espace.library.uq.edu.au/view/UQ:40848>
39. El Nabahany, U., Mosbech, A.-M., Mgeni, M., & Yunus, S. (2019). *A Transformation into Digitally Supported Education: Case from the State University of Zanzibar*.
40. In A. Tamall & N. Mavengere (Eds.), *Sustainable ICT, Education and Learning* (pp. 16–23). Springer International Publishing. https://doi.org/10.1007/978-3-030-28764-1_3
41. Enon, J. C. (1998). *Education Research Statistics and Measurement*. Kampala. Makerere University Press. - Google Search.
42. Fromkin, V., Rodman, R., & Hyams, N. (2018). *An Introduction to Language*. Cengage Learning. [https://books.google.com/books?hl=en&lr=&id=idQWAAAAQBAJ&oi=fnd&pg=PR5&dq=Fromkin,+Rodman+and+Hyams+\(2003\)&ots=d3QF0s7n_X&sig=_94gvirq0z1lo2zSVO3685KyAJw](https://books.google.com/books?hl=en&lr=&id=idQWAAAAQBAJ&oi=fnd&pg=PR5&dq=Fromkin,+Rodman+and+Hyams+(2003)&ots=d3QF0s7n_X&sig=_94gvirq0z1lo2zSVO3685KyAJw)
43. Garfias, R. (2004). *Music: The Cultural Context* (Vol. 47). National Museum of Ethnology Osaka.
44. Gitonga, N. (2017). *Uchambuzi Linganishi Wa Fani Na Maudhui Ya Nyimbo Za Harusi Za Kimeru Na Za Kiswahili* [Thesis, University of Nairobi]. (Haijachapishwa). <http://erepository.uonbi.ac.ke/handle/11295/101711>
45. Graebner, W. (1991). *Taarab-Populäre Musik am Indischen Ozean, Populäre Musik in Afrika*. Veit Erlmann. Vol 1. 181-200. - Google Search. [https://www.google.com/search?rlz=1C1S0JL_enKE889KE889&q=Graebner,+W.+\(1991\).TaarabuPopulare+Musik+am+Indischen+Ozean,+Populare+Musik+in+Afrika.+Veit+Erlmann.+Vol+1.+181200.&sa=X&ved=2ahUKewj6mNmHzL72AhUR3hoKHxmA9EQgwN6BAGBEAE&csid=1647020175058452](https://www.google.com/search?rlz=1C1S0JL_enKE889KE889&q=Graebner,+W.+(1991).TaarabuPopulare+Musik+am+Indischen+Ozean,+Populare+Musik+in+Afrika.+Veit+Erlmann.+Vol+1.+181200.&sa=X&ved=2ahUKewj6mNmHzL72AhUR3hoKHxmA9EQgwN6BAGBEAE&csid=1647020175058452)
46. Graebner, W. (2004). *Between Mainland and Sea: The Taarab Music of Zanzibar*. In *Isl and Musics*. Routledge.
47. Gunderson, F. D., & Barz, G. F. (2000). *Mashindano!: Competitive Music Performance in East Africa*. Mkuki na Nyota Publishers.
48. Harries, L. (1962). *Swahili Poetry*. Nairobi. OUP. <https://www.worldcat.org/title/swahilipoetry/oclc/307457>
49. Hassan, A. H. (2017). *Kuchunguza Fasihi ya Majina ya Mitaa Mjini Unguja. Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu cha Huria cha Tanzania*. <http://repository.out.ac.tz/2203/1/TASNIFU%20-%20HALIMA%20ALI%20HASSAN.pdf> (haijachapishwa). 194
50. Herms, D. I. (2012). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Toleo la Pili*. [A Standard Swahili Dictionary. Second edition]. Nairobi: Oxford University Press. xviii, 477 pp. ISBN 0195732227. (Ca. 15000 ThS/ 15.- €). Swahili-Forum - 12.2005. <https://nbn-resolving.org/urn:nbn:de:bsz:15-qucosa-91314>
51. Isabelle, D. N. (2016). *Interpreting Metaphor: Perspectives From Pragmatics and Psychology*. *Tasnifu ya Uzamifu Chuo Kikuu cha London*.
52. Isabelle, R. (2017). *Metaphors in English for Law: Let Us Keep Them*. University Jean Moulin-Lyon3. https://www.researchgate.net/publication/305849253_Metaphors_in_English_for_Law_Let_Us_Keep_The_m

53. I-Wensu, L. (2002). "What About Culture can Metaphor Tell us?" *National Taiwan University Language and Linguistics*. 3: 3: 589-612. - Google Search. http://homepage.ntu.edu.tw/~gilntu/Faculty/Lily_I-Wen_Su.html
54. Jahadhy, A. (1966). *Waimbaji wa Juzi. Dar es Salaam. Chuo cha Uchunguzi wa Lughaya Kiswahili*. - Google Search. <https://www.hrw.org/sw/news/2020/11/22/377089>
55. Jilala, H. (2008). *The Artistic Uses of Metaphors in Constructing Meanings and Messages in new Generation Songs in Tanzania [Masters, The Open University of Tanzania]*. [http://repository.out.ac.tz/169/\(haijachapishwa\)](http://repository.out.ac.tz/169/(haijachapishwa)).
56. Juma, N. H. (2016). *Kuchunguza Fani na Dhamira katika Semi Zilizoandikwa katika Vyombo vya Safari vya Baharini Kisiwani Pemba [Masters, The Open University of Tanzania]*. [http://repository.out.ac.tz/1836/\(haijachapishwa\)](http://repository.out.ac.tz/1836/(haijachapishwa)).
57. Kahigi, K. K., & Mulokozi, M. M. (1982). *Kunga za Ushairi na Diwani ya Yetu. Dar es Salaam. Tanzania Publishing House*. <https://www.worldcat.org/title/kunga-zaushairi-na-diwani-yetu/oclc/10779087195>
58. Kaneko, M., & Sutton-Spence, R. (2012). *Iconicity and Metaphor in Sign Language Poetry. Metaphor and Symbol*, 27(2), 107–130. <https://doi.org/10.1080/10926488.2012.665794>
59. Kea, K. (2006). *A Study for the European Commission on the Economy of Culture (2006). Culture Action Europe*. <https://cultureactioneurope.org/knowledge/creativesindustries/1-the-economy-of-culture-in-europe/>
60. Kea, P. (2011). *Usemezo katika Nyimbo za Taarab [Thesis]*. <https://irlibrary.ku.ac.ke/handle/123456789/1931> (haijachapishwa).
61. Khamis, A. (1981). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Nairobi. Oxford University Press*. <https://www.worldcat.org/title/kamusi-ya-kiswahili-sanifu/oclc/9219392>
62. Khamis, A. M. (2012). *Matumizi ya Mafumbo na Taswira katika Nyimbo za Mapenzi za Taarab Asilia ya Zanzibar [PhD Thesis]. University of Dar es salaam*(haijachapishwa).
63. Khamis, W. A. (2016a). *Kuchunguza Dhamira za Nyimbo za Siti Bint Saad [Masters, The Open University of Tanzania]*. [http://repository.out.ac.tz/1835/\(haijachapishwa\)](http://repository.out.ac.tz/1835/(haijachapishwa)).
64. Khamis, S. M. A. (2016). *Versality of the Taarab Lyric: Local Aspect and Global Influences. Swahili Forum 11: 3-37*.
65. Khatib, M. S. (1992). *Taarab Zanzibar. Tanzania Pub. House*.
66. Kibao, M. S. (1983). *Namma ya Kujifunza, Kuliandika na Kulifumbua Shairi la Kiswahili*.
67. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili III: 96-113. King'ei, G. K. (1993). *Language, Culture and Communication: The role of Swahili*
68. *Taarab songs in Kenya, 1963-1990 - ProQuest*. <https://www.proquest.com/openview/223bad5e61cbea4c905c0e4e6435b977/1?pq-origsite=gscholar&cbl=18750&diss=y>
69. King'ei, K. G., & Amata, J. K. (2001). *Taaluma ya Ushairi. Acacia Stantex Publishers*. <http://books.google.com/books?id=JqcaAQAIAAJI96>
70. King'ei, K. G., & Kisovi, C. N. M. (2005). *Msingi wa Fasihi Simulizi. Kenya Literature Bureau*. <https://www.worldcat.org/title/msingi-wa-fasihi-simulizi/oclc/67241367>
71. Kipacha, A. (2015). *Taswira za Ndege katika Maandiko ya Shaaban Robert. SwahiliForum 22 (2015), 22, 1–19*.
72. Kobia, M. J. (2016). *A conceptual Metaphorical Analysis of Swahili Proverbs with reference to Chicken Metaphor. Internationa Journal of Education and Research*. 4: 217-227
73. Kothari, C. R. (1990). *Research Methodology Methods And Techniques*. <https://pdfcookie.com/documents/research-methodology-methods-andtechniques-by-cr-kothari-7rv3wzk460ld>
74. Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques. New Age International*. [https://books.google.co.ke/books?hl=en&lr=&id=hZ9wSHysQDYC&oi=fnd&pg=PA2&dq=Kothari,+R.+\(1992\).+Research+Methodology:+Methods+and+Techniques.+New+Delhi.+New+Age+International+Ltd.&ots=1tXenHc4C5&sig=txcbGhHZ7U0q9iT_TqG1KFAQSc4&redir_esc=y#v=onepage&q&f=false](https://books.google.co.ke/books?hl=en&lr=&id=hZ9wSHysQDYC&oi=fnd&pg=PA2&dq=Kothari,+R.+(1992).+Research+Methodology:+Methods+and+Techniques.+New+Delhi.+New+Age+International+Ltd.&ots=1tXenHc4C5&sig=txcbGhHZ7U0q9iT_TqG1KFAQSc4&redir_esc=y#v=onepage&q&f=false)
75. Koul, H. L. (2009). *Large Sample Inference for Long Memory Processes. World Scientific Publishing Company*.
76. Kull, K. (2003). *Semiotics Is a Theory of Life. Semiotics, 15–31*. <https://doi.org/10.5840/cpsem200337>
77. Lakoff, G., & Johnson, M. (1980). *Metaphors we live by. Chicago. University of Chicago Press*. https://www.cc.gatech.edu/classes/AY2013/cs7601_spring/papers/Lakoff_Johnson.pdf
78. Lakoff, G., & Johnson, M. (2003). *Metaphors We Live By (W. a new Afterword, Ed.). University of Chicago Press*. <https://press.uchicago.edu/ucp/books/book/chicago/M/bo3637992.html197>
79. Lange, S. (2000). *Muungano and TOT: Rivals on the Urban Cultural Scene. CMI - Chr. Michelsen Institute*. <https://www.cmi.no/publications/989-muungano-and-tot>
80. Leech, G. (2008). *Language in Literature: Style and Foregrounding. Routledge*. <https://doi.org/10.4324/9781315846125>
81. Leech, G., Hoogenraad, R., Birch, D., & Birch, D. (1984). *English Grammar for Today: A New Introduction. RELC Journal, 15(2), 95–100*. <https://doi.org/10.1177/003368828401500208>

82. Leech, G. N. (1969). *A Linguistic Guide to English Poetry*. Routledge & CRC Press. <https://www.routledge.com/A-Linguistic-Guide-to-EnglishPoetry/Leech/p/book/9780582550131>
83. Madumulla, J. S. & Mlacha, S. A. K. (1991). *Riwaya ya Kiswahili. Dar es Salaam Univ.Press.* <https://www.worldcat.org/title/riwaya-ya-kiswahili/oclc/246712174>
84. Maitaria, N. J. & Wafula, R. M. (2018). *Ushairi wa Abdilatif Abdalla katika Kubainisha Utamaduni wa Waswahili. Journal Of Linguistics and Language in Education.* Juzuu la 12: 2: 74-92.
85. <https://karospace.karu.ac.ke/bitstream/handle/20.500.12092/2283/Maitaria%202018.pdf?sequence=1&isAllowed=y>
86. Makilla, S. (2011). *Taarab Asili ni Urithi Usiostahili Kupotea.* <http://jitambueafrika.blogspot.com/2011/06/taarab-asilini-urithi-usiostahili.html>
87. Masinde, E. (1992). *Mashairi Huru: Uchambuzi wa Dhamira na Mtindo. Tasnifu ya M.A.Chuo Kikuu Cha Kenyatta (haijachapishwa).*
88. Mbaabu, I. (1985). *New Horizons in Kiswahili: A Synthesis in Developments, Research, and Literature.* Kenya Literature Bureau.
89. McHoul, A. (2003). *Review: Understanding Media Semiotics, Ethnographic Research for Media Studies. Media International Australia, 106(1), 153–156.* <https://doi.org/10.1177/1329878X0310600116>
90. Mgana, I. (1991). *Jukwaa la Taarab-Zanzibar. Maailman musiikin instituutti.*
91. Mnenuka, A. (2012). *Tofauti ya Dhana ya Mwanamke katika Jamii: Mifano kutoka katika Taarab (mipasho) na Nyimbo za Kibena. Swahili Forum.* https://www.academia.edu/3333326/Tofauti_ya_dhana_ya_mwanamke_katika_jamii_mifano_kutoka_katika_taarab_mipasho_na_nyimbo_za_kibena
92. Mohamed, M. A., & Mohamed, S. A. (1998). *Kamusi ya Visawe. East African Publishers.*
93. Mohamed, S. A. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili: Tamthilia, Riwaya, na Hadithi Fupi. East African Educational Publishers.* <https://www.worldcat.org/title/kungaza-nathari-ya-kiswahili-tamthilia-riwaya-na-hadithi-fupi/oclc/35948754>
94. Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi. East African Educational Publishers.* <http://catalog.hathitrust.org/api/volumes/oclc/38526645.html>
95. Mulokozi, M. M. (1996). *Kioo cha Lugha.* <https://www.ajol.info/index.php/kcl/about/submissions>
96. Mulokozi, M., & Mugyabuso, M. (1999). *Tenzi Tatu za Kale. In Wikipedia, Kamusi Elezo Huru.* https://sw.wikipedia.org/w/index.php?title=Tenzi_tatu_za_kale&oldid=1149488
97. Mwalagho, E. (2007). *Taarab and Chakacha in East Africa: Transformation, Appreciation and Adaptation of Two Popular Music Genres of the Kenyan Coast.* https://www.academia.edu/35556240/Taarab_and_Chakacha_in_East_Africa_Transformation_Appreciation_and_Adaptation_of_Two_Popular_Music_Genres_of_the_Kenyan_Coast
98. Mwamzandi, I. Y. (2007). *Utandawazi na Teknolojia ya Mawasiliano katika Umalenga wa Waswahili: Mfano wa Sitiari za Taarab. Elimu Nchini Kenya. 1: 68-82.*
99. Mwamzandi, I. Y. (2014). *Swahili; Computational Ling, Pragmatics, Text/Corpus Ling: Swahili Word Order Choices. The Linguist List.* <https://linguistlist.org/issues/25/25-2854.html199>
100. Mwangi, P. K., & Munyao, J. K. (2017). *Mtindo na Maudhui katika Nyimbo za Kistasaza Msanii John De'Mathew nchini Kenya. Mulika Journal, 35(1), Article 1.* <https://journals.udsm.ac.tz/index.php/mj/article/view/758>
101. Mzee, N. (2011). *Athari za Nyimbo za Mipasho kwa Jamii ya Wanzanzibar. Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu Cha Huria Cha Tanzania (haijachapishwa).*
102. Nadra, S. K. (2017). *Mabadiliko katika Nyimbo za Taarab na Uwasilishaji wake Kulingana na Wakati. Tasnifu ya M. A Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.* <http://repository.udom.ac.tz/bitstream/handle/20.500.12661/453/NADRA%20SOUD%20-%20RIPOTI.pdf?sequence=1&isAllowed=y> (haijachapishwa).
103. Nasra, M. H. (2007). *African Books Collective: Mfyanzi Aingia Kasri.* <https://www.africanbookscollective.com/books/mfnyanzi-aingia-kasri.-siti-bintsaad-malkia-wa-taarab>
104. Nasrul, S. (2018). *The Functions of Metaphor in the Lyrics of Rayolas Song. International Journal of Humanity Studies (IJHS), 2(1), 61–69.* <https://doi.org/10.24071/ijhs.v2i1.763>
105. Ngonyani, D. (2005). *Vitendawili vya Kiswahili : Usambamba wake na Dhima katika Jamii. Swahili Forum. 12: 121-132.*
106. Nguti, M. (2013). *Ulinganishi wa Matumizi ya Tasfida za Mukadha wa Nyumbani katika Lugha ya Kikamba na Kiswahili [Thesis].* <http://erepository.uonbi.ac.ke/handle/11295/60185> (haijachapishwa).
107. Njogu, K., & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu Nairobi Jomo.* <https://www.coursehero.com/file/p7tfdjt/Njogu-K-na-Chimerah-R-1999-Ufundishaji-wa-Fasihi-Nadharia-na-Mbinu-Nairobi-Jomo/>
108. Nkonga, M. (1988). *Literacy Study of Joseph Kamaru: Theme and Style. Tasnifu ya M.A.Chuo Kikuu cha Nairobi (haijachapishwa).* 200
109. Ntarangwi, M. (1998). *Swahili, Taarab, Zanzibar. Trenton Asmara. Text Production Frauen.*

<https://www.grafiati.com/en/literature-selections/swahili-taarabzanzibar-textproduktion-frauen/dissertation/>

110. Ntarangwi, M. (2001). Cultural Analysis, A Socio-Historical and Contextual Analysis of Popular Musical Performance Among the Swahili of Mombasa, Kenya.